UCHAMBUZI WA BAJETI YA SEKTA YA KILIMO, NA UWIANO KATIKA MATUMIZI YA FEDHA ZA MFUKO WA MAENDELEO KWA WANAWAKE NA VIJANA: HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO, TANZANIA

Ripoti ya Utafiti kwa Muhtasari

1. UTANGULIZI

Muhtasari huu unaelezea matokeo ya zoezi la uchambuzi wa bajeti ya sekta ya kilimo lililofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo (HWK) Februari 2019. Mchanganuo huo ulilenga masuala ya uwiano—jinsi uhusiano kati ya madaraka, utoaji maamuzi na bajeti vinavyoweza kuingizwa katika uandaaji na utekelezaji wa sera na bajeti kwa kuzingatia mahitaji na maslahi ya wakulima wadogo, hasa wanawake na vijana ili yaweze kushughulikiwa ipasavyo. Mwongozo wa Wizara ya Fedha na Mipango unazitaka Mamlaka ya Serikali za Mitaa Tanzania Bara kuelekeza 20% ya mapato ya ndani yatokanayo na shughuli za kilimo kutumika katika kuendeleza sekta hiyo. Aidha 15% kwenda mifugo na 5% kuendeleza sekta ya uvuvi. Kadhalika, kila Halmashauri imeagizwa kutenga 10% kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya wanawake (4%), vijana (4%) na watu wenye ulemavu (2%). Maagizo haya yako sanjari na Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025, Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na Uhakika wa Chakula Tanzania (TAFSIP) na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya II (2016/17-2020/21). Lengo la uchambuzi wa bajeti za Mwaka wa Fedha (MF) 2013/14 hadi 2017/18 ni kuwataarifu watendaji wa Halmashauri, madiwani na wadau mbali mbali kuhusu vipaumbele katika bajeti na matumizi ya fedha za Halmashauri katika kuendeleza sekta ya kilimo, mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa bajeti, na kuchangia mawazo yanayoweza kuboresha sera na mfumo wa ugawaji wa rasilimali za umma unaozingatia uwiano wa kijinsia.

2. MBINU YA UTAFITI

Takwimu zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbali mbali za kitafiti ikiwemo mahojiano na viongozi wa Halmashauri na kupitia, kuhakiki na kuchambua kwa kina taarifa na ripoti za fedha za Halmashauri, Mipango na Mfumo wa Matumizi kwa Kipindi cha muda wa kati, yaani miaka mitatu (MTEF) ulifanywa kwa miaka sita ya fedha mfululizo kutoka 2013/14 hadi 2018/2019.

3. MATOKEO MUHIMU

3.1. Kiasi cha fedha zilizotengwa kwa sekta ya kilimo

HWK imekuwa ikitengewa mgawo mdogo wa bajeti ya kilimo kwa miaka sita mfululizo, kutoka MF 2013/14 hadi 2018/19 na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kilimo wilayani. Katika MF 2013/14 kwa mfano, kilimo kiliidhinishiwa TSH 1.4 bilioni, sawa na 5.9% ya bajeti yote ya HWK, lakini mgawo wa sekta hiyo ulipungua hadi 4.7% mnamo 2014/15. Sehemu ya bajeti ya kilimo katika bajeti ya jumla ya Halmashauri ilishuka hadi kufikia 2.9% katika kipindi cha MF 2015/16.

Ongezeko kwenye bajeti ya kilimo lilionekana MF 2016/17 japo mwaka mmoja baadaye, mgawo kwa sekta hiyo ulipunguzwa kutoka 6.0% (2016/17) hadi 4.6% MF 2017/18. Katika bajeti ya 2018/19, sekta ya kilimo ilitengewa TSH 1.4 bilioni, ambayo ni sawa na jumla ya bajeti ya sekta hiyo iliyotengwa miaka mitano kabla, yaani mwaka 2013/14. Ongezeko la kila mwaka la bajeti ya kilimo lilisimama kwa miaka sita iliyopita, isipokuwa 2016/17 ambapo mgawo kwa sekta hiyo ulikua kwa zaidi ya mara mbili (Angalia Jedwali 1). Ongezeko hili lilitokana na ongezeko kubwa la bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa HWK wanaofanya kazi kuendeleza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi—kutoka TSH 1.0 bilioni MF 2015/16 hadi karibu TSH 2.2 bilioni MF 2016/17.

Jedwali 1: Mwenendo bajeti halisi na mgao wa kilimo katika HWK 2013/14 -2018-2019

Mwaka wa Fedha	Jumla ya bajeti ya HWK (mamillioni ya TSH)	Jumla ya mgawo wa kilimo (mamillioni ya TSH)	% ya ongezeko la bajeti ya kilimo	% ya bajeti ya kilimo kwa bajeti ya wilaya	% badiliko katika mgawo
2013/14	24,359.3	1,428.4		5.9	
2014/15	28,740.3	1,354.0	-5.2	4.7	-1.2
2015/16	39,719.0	1,167.4	-13.8	2.9	-1.8
2016/17	41,667.4	2,483.4	112.7	6.0	3.0
2017/18	45,377.6	2,072.7	-16.5	4.6	-1.4
2018/19	34,808.9	1,422.3	-31.4	4.1	-0.5

Chanzo: HWK Idara ya Mipango, Februari 2019

3.2. HWK inavyogawa bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo katika sekta ya kilimo

Bajeti ya kilimo iliyotengwa kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa miaka sita iliyopita inaonesha kuwa sehemu ya bajeti ya sekta hiyo inayoenda katika maendeleo ni ndogo licha ya juhudi za serikali kupunguza gharama za kiutawala. Kwa MF 2013/14, sehemu ya bajeti ya kilimo iliyotengwa kwa maendeleo ilikuwa 26.9%, na mwaka mmoja baadaye mgawo uliongezwa hadi 30.5% (MF 2014/15). Walakini, sehemu ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya kilimo ilipunguzwa sana kuwa 6.9% mnamo 2015/16 na iliongezeka tu hadi 11.9% mnamo 2018/19. Kwa kuzingatia takwimu hizi, ni sahihi kusema kwamba HWK haitoi kipaumbele kwa sekta ya kilimo katika matumizi yake ya maendeleo.

3.3. Vyanzo vikuu vya fedha kwa ajili ya bajeti ya kilimo katika HWK

HWK inapata mapato yake kutoka vyanzo vikuu vinne: (i) serikali kuu (CG), (ii) Wahisani wa Maendeleo, (iii) mikopo na (iv) vyanzo vya ndani ya Halmashauri. Halmashauri hukusanya mapato yake kutoka kwenye vyanzo kama vile ushuru wa mazao, kodi ya ardhi, ushuru wa huduma, ada ya maombi ya zabuni, ushuru wa hoteli, mazao ya misitu, ada ya mabasi, uuzaji wa viwanja na majengo, leseni mbali mbali, ada na malipo. Mchanganuo unaonesha kuwa bajeti ya kilimo wilayani Kilolo inategemea sana ruzuku kutoka serikali kuu. Kwa wastani, serikali kuu ilichangia 90.8% ya jumla ya bajeti yote ya kilimo katika kipindi kati ya 2013/14 na 2018/19. Halmashauri ilichangia 6.6% tu ya bajeti ya jumla, na 2.6% ya fedha hutoka kwa wahisani na wadau mbali mbali wa maendeleo (Angalia Jedwali 2).

Jedwali 2: Bajeti ya kilimo HWK kufuatana na vyanzo vya mapato 2013/14-2018/19

Mwaka wa Fedha	Jumla ya bajeti ya kilimo (mamillioni ya TSH)	Mgao toka Hazina		Mapato ya ndani		Wahisani	
		Kiasi	%	Kiasi	%	Kiasi	%
2013/14	1,428.5	1,415.0	99.1%	13.4	0.9%	0	0.0%
2014/15	1,354.1	1,333.2	98.5%	20.8	1.5%	0	0.0%
2015/16	1,167.4	1,087.4	93.1%	80.0	6.9%	0	0.0%
2016/17	2,581.3	2,193.6	85.0%	289.7	11.2%	98.0	3.8%
2017/18	2,297.3	2,072.7	90.2%	104.4	4.5%	120.0	5.2%
2018/19	1,472.2	1,252.8	85.1%	169.4	11.5%	50.0	3.4%
Jumla kuu	**10,300.8**	**9,354.9**	**90.8%**	**677.9**	**6.6%**	**268.0**	**2.6%**

Chanzo: Idara ya Mipango, HWK, Februari 2019

Kwa miaka sita iliyopita, jumla ya TSH 5.1 bilioni zilitengwa kusaidia shughuli za maendeleo ya kilimo HWK. Kati ya mgawo huo, zaidi ya 50% ilitoka kwenye mfuko wa maendeleo wa kilimo cha umwagiliaji/ mpango mdogo wa kuendeleza umwagiliaji (TSH 2.5 bilioni) ikifuatiwa na ruzuku ya maendeleo ya kilimo/ ruzuku ya kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa (30.1%), vyanzo vya ndani ya Halmashauri (13.1%), Programu ya Usimamizi wa Uhifadhi ya Kihansi (5.3%), na ruzuku (1.2%) ya kujenga uwezo (Angalia Mchoro 1). Eneo la kipaumbele kwa matumizi kutoka MF 2013/14 hadi 2018/19 lilikuwa ujenzi/matengenezo ya miundombinu ya umwagiliaji ikichukua 72.3% ya matumizi yote halisi (kwa miaka yote).



Kielelezo 1: Matumizi kwa kutoa kipaumbele katika kilimo HWK

Maeneo mengine ya matumizi kama maonesho ya kilimo yalichukua 24.2% wakati ujenzi wa uwezo ulichota 3.5% ya matumizi yote. Kwa miaka mitano iliyopita, Halmashauri haikuingiza fedha zozote za kuboresha uwezo wa wafanyakazi wa ugani, upatikanaji wa pembejeo za kilimo na mitambo ya kilimo. Mwongozo wa bajeti juu ya mgawo wa 20% unaotokana na pato la ndani ya Halmashauri kwa kilimo, 15% kwa mifugo na 5% kwa uvuvi haukutekelezwa

3.4. Tathmini ya mgawo wa 10% kwa MMWV na mchango wake katika kilimo

Serikali ya Tanzania ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana (MMWV) ili kushughulikia mapungufu katika uwiano, na kuwawezesha wanawake na vijana kujihusisha na kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi. Serikali iliagiza kila Halmashauri kutenga 4% ya mapato ya ndani kwa ajili ya wanawake, nyingine 4% kwa vijana na 2% kwa watu wenye ulemavu. Hivi karibuni serikali ilianzisha ukaguzi maalumu wa MMWV ambapo kutotenga 10% ni "kosa la jinai."

Kuanzia 2013/14 hadi 2018/19, HWK ilitenga jumla ya TSH 201.5 milioni kwa ajili ya MMWV, sawa na 1.5% ya jumla ya makusanyo ya ndani. Taarifa ya 2013/14 haijaonesha mgawo wowote lakini mnamo 2014/15, Halmashauri iliweka TSH 4.5 milioni (0.2%) kwa MMWV. Tangu wakati huo, HWK imekuwa ikigawa kila mara fedha kwa MMWV. Mwaka 2015/16 mgawo huo ulikuwa TSH 13.0 milioni (0.6%) na uliongezwa hadi milioni 18.0 (0.8%) mnamo 2016/17. Lakini mgawo kwa MMWV ulipunguzwa tena hadi kufikia TSH 16 milioni (0.6%) mwaka 2017/18. Wakati pekee ambapo HWK iligawa kiasi kikubwa cha fedha kwa MMWV ni MF 2018/19 ambapo malipo yote yalikuwa TSH 150.0 milioni ambayo ni sawa na 9.2% ya jumla ya makusanyo toka vyanzo vya ndani mwishoni mwa Februari 2019 (Angalia Jedwali 3).

Jedwali 3: Mgawo wa bajeti kwa MMWV katika mamilioni ya TSH, mwaka 2013 / 14- 2018/19

Mwaka	Jumla ya pato la ndani (Halisi) (Mamilioni ya TSH)	Matumizi yaliyoidhin-ishwa MMWV	Kiasi kilichopelekwa MMWV	% toka pato la ndani kwenda MMWV	Matumizi halisi	% ya matumizi ya kiasi halisi kilichotolewa
2013/14	2,965.6	0.0	0.0	0.0%	0.0	Hakuna
2014/15	1,923.3	96.2	4.5	0.2%	4.5	100.0%
2015/16	2,180.1	241.5	13.0	0.6%	13.0	100.0%
2016/17	2,319.5	290.2	18.0	0.8%	18.0	100.0%
2017/18	2,784.5	290.0	16.0	0.6%	16.0	100.0%
2018/19*	1,628.1	241.6	150.0	9.2%	0.0	0.0%
Total	**13,801.1**	**1,159.4**	**201.5**	**1.5%**	**51.5**	**25.5%**

Chanzo: Idara ya Maendeleo ya Jamii, HWK – Februari 2019; * Mpaka Februari 2019

Matokeo haya yanaonesha kuwa HWK haijatekeleza vyema mwongozo wa serikali wa kutenga 10% kwa MMWV. Kwa MF 2016/17 pekee, Halmashauri ilishindwa kutoa zaidi ya TSH 97 milioni kwa hivyo kiasi cha fedha ambazo hazikutolewa ziliongezeka hadi TSH 262.4 milioni mwaka 2017/18. Inadaiwa kuwa sababu kuu za kutoweza kutimiza wajibu wa kisheria ni pamoja na kucheleweshwa kwa malipo mengineyo (OC) na ruzuku kutoka Serikali Kuu ambayo inalazimisha Halmashauri kutumia sehemu ya mapato yake ya ndani kulipia gharama ya shughuli za uendeshaji. Mahojiano na maafisa wa Halmashauri yalibainisha kuwa serikali kuu imeondoa vyanzo kadhaa vya mapato ya Halmashauri kama ushuru wa mali, mabango na ada ya maegesho ambayo huwa ni vyanzo vikuu vya mapato ya ndani. Mtu mmoja aliyehojiwa alisema: *"... Mamlaka ya Serikali za Mitaa pia zinapoteza makusanyo mengi kufuatia kuanzishwa kwa Vitambuisho vya Wamachinga."*

3.5. Usambazaji wa mgawo wa MMWV kati ya wanawake na vijana

Katika MF 2014/15 mgawo wa MMWV ulifanyika kwa usawa kati ya wanawake na vijana. Mwaka 2015/16 sehemu kubwa ya fedha zilikwenda kwa vijana (76.9%) ikilinganishwa na wanawake (23.1%), kadhalika MF 2016/17 ambapo karibu 78% ya fedha za mfuko huo walipewa vijana. Mbali na mgawo wa MMWV, vijana pia walipokea jumla ya TSH 29 milioni mwaka 2014/15, na TSH 10 milioni mnamo 2016/17 kutoka wizara inayohusika na maendeleo ya vijana, ikifanya vijana kuwa wanufaika wakubwa zaidi wa mfuko wa maendeleo.

Mwaka 2017/18 zaidi ya theluthi mbili ya mgawo wa MMWV ulikwenda kwa wanawake (68.8%) ikilinganishwa na vijana (31.3%). Katika kipindi hicho hicho, vijana walipokea nyongeza ya TSH 13 milioni

kutoka kwa Wizara ya Maendeleo ya Vijana na Michezo. Haikuwekwa bayana ni kiasi gani cha mgawo ulikwenda kwa watu wenye ulemavu. Hii inaonesha kuwa, isipokuwa mwaka 2014/15, miongozo ya serikali juu ya uwezeshaji wa MMWV haikuzingatiwa vizuri. Jumla ya vijana 133 (vikundi 24 vya kiuchumi walipata TSH 31.2 milioni) na wanawake 179 (vikundi tisa vya kiuchumi) walifaidika na MMWV tangu 2014/15.

3.6. Jinsi WYDF ilivyotumika

Sehemu kubwa ya MMWV ilitumiwa kwenye shughuli zinazohusiana na kilimo (Angalia Mchoro 2).



Mchoro 2: Jinsi MMWV ilivyotumiwa katika HWK

4. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

4.1. Hitimisho

Kwa miaka sita iliyopita (2013/14 hadi 2018/19), bajeti ya kilimo imetawaliwa na ucheleweshwaji na kutotabirika kwa mgawo wa fedha. Makusanyo ya ndani ya Halmashauri kwenda sekta hiyo imekuwa chini sana kuliko kiwango kilichowekwa katika miongozo ya bajeti. Hata MMWV ambayo inatarajiwa kukuza ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo chenye tija imetengewa rasilimali chache kuliko maagizo ya kisheria ya 10%. Ni katika MF 2018/19 ambapo tunaona ongezeko kubwa la mgawo kwa MMWV. Hata hivyo, ongezeko hili halitaweza kuleta matokeo yanayotarajiwa hadi masuala kadhaa yatakaporekebishwa ikiwemo ukosefu wa fedha za kujenga uwezo; kuingiliwa na siasa katika usimamizi wa MMWV; matumizi ya fedha kwa upande wa vikundi vya walengwa na kiwango cha ufanisi wa urejeshaji wa mikopo.

4.2. Mapendekezo

Ili kushughulikia baadhi ya changamoto hizi, yafuatayo yanapendekezwa:

- Serikali kuu inapaswa kupitia upya na kuboresha sera za kodi na ushuru katika serikali za mitaa na kuimarisha utekelezaji wa miongozo ya bajeti juu ya mgawo wa 20% wa mapato ya Halmashauri kwenda kuendeleza kilimo, 15% kusaidia sekta ya mifugo na 5% kuwekeza katika uvuvi.
- Serikali inapaswa kutoa miongozo ya kusimamia mfuko maalumu wa maendeleo kwa vijana na watu wenye ulemavu na kupitia upya miongozo ya sasa ya 10% ya bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo, kusimamia, kufuatilia na kutathmini.
- Kuna haja ya kuoanisha michakato ya maombi ya mikopo na usimamizi wa MMWV na Mifuko ya Waziri ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri na uwajibikaji wakati wa kuomba na kutumia mikopo.

Imetafsiriwa na Mbarwa Kivuyo
Imehakikiwa na Magreth Henjewele
©ANSAF & SAIRLA, Septemba 2019

Rejea
Magreth Henjewele (2019) Uchambuzi wa Bajeti ya Sekta ya Kilimo, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Tanzania. Taarifa imeandaliwa kwa ajili ya Jukwaa la Kitaifa wa Kujifunza kuhusu Kilimo Shadidi Endelevu nchini Tanzania kuhusu Kilimo Shadidi Endelevu, Juni 2019. ANSAF. SAIRLA. Pakua taarifa kamili kwa kubofya: https://sairla-africa.org/wp-content/uploads/2019/08/Kilolo-DC-Budget-Analysis-Study_FINAL.pdf